# KUFUNGUA MIUJIZA YA KIFEDHA KATIKA MAISHA YAKO

Unaweza kufungua muujiza wa kifedha katika maisha yako?

Utakaposoma kanuni zifuatazo sita , utaona vile Mungu anaweza kutukidhi na kututengenezea njia.

Siamini kuwa utashuhudia miuzuja ya kifedha hadi uzifanyize kazi hoja nitakazoshiriki nanyi kutoka neno la Mungu.

Njia ya kwanza ya kuufungua muujiza wa kifedha ni kupitia:

USIMAMIZI WA HEKIMA CHINI YA UONGOZI WA MUNGU

Tuyaangalie maisha ya Yusufu.Yusufu alijua maisha yake yalikuwa mikononi mwa Mungu na kibali cha Mungu kilikuwa juu yake alipokuwa akimuinua Yusufu .Ulifika wakati Yusufu aliitwa na Farao akamfasiria ndoto yake.Tafsiri ya ndoto ile ilikuwa kungekuwa na miaka saba ya shibe na miaka saba ya njaa. Mungu aliwafunulia watu kile ambacho kingefanyika ili wajiandae .

Mungu huwafunulia watu wake mipango yake, wale wanaomtafuta ili wapate hekima. Wataipata na Mungu hataizuia kulingana na Yakobo 1. Ukitafuta hekima katika awamu ya kifedha , jua kuwa miujiza hii haipatikani tu .Miujiza katika awamu hii ya kifedha lazima iendelezwe kulingana na mpango wa Mungu na kusudi lake.

Hili ndilo lilikuwa wazo la Yusufu kwa Farao .

"*Basi Farao ajitafutie mtu wa akili na hekima amweke juu ya nchi ya Misri .Farao na afanye hivi, tena akaweke wasimamizi juu ya nchi, na kutwaa sehemu ya tano katika kila nchi ya Misri , katika miaka hii saba ya kushiba* "(mwanzo 41:33-34).

Hii inamaanisha kuwa wakati wa miaka ile saba ya shibe , wangechukua sehemu ya tano ya kile kilikuwa kikikua na kukiweka kando kisha kukiweka kwa ajili ya miaka ile saba ya njaa.Huu ulikuwa usimamizi mzuri na wa hekima wa rasilimali zao.Usichukue kila unachomiliki na kukitumia .Bakiza angalau uweze kupanda tena.Hili ni jambo muhimu sana.

Mkulima akitumia kila kitu kinachotokana na mavuno yake na akose kupanda tena ,kutafanyikaje wakati wa kupanda ukifika?Hatakuwa na mbegu za kupanda ili apate mazao mapya .

Tunatakiwa kuwa wasimamizi wenye hekima wakati Mungu anaelekeza na kukarimia.

"*Na wakusanye chakula chote cha miaka hii myema ijayo , waweke akiba ya nafaka mkononi mwa Farao wakakilinde chakula katika miji.Na hicho chakula kitakuwa akiba kwa ajili ya miaka hiyo saba ya njaa, itakayokuwa katika nchi ya Misri ,nchi isiharibike kwa njaa.Neno hilo likawa njema machoni pa Farao akawambia watumwa wake "tupate wapi mtu kama huyu, mwenye roho ya Mungu ndani yake?"(*mwanzo 41:35-38).

Tazama Mungu aliinuliwa katika nchi yote kupitia uwongozi. Kwa nini walifanya hivyo? Kwa sababu Farao alijua kuwa Yusufu alisikia kutoka kwa Mungu .Naamini kuwa, sisi kama watu wa Mungu ikiwa tunataraji kuiona muujiza ya kifedha katika maisha yetu,tunahitaji kusikia kutoka kwa Mungu .Tunatakiwa kuomba tukimjulisha Mungu tukitakacho bayana.

Mwombe ukitakacho hasa Bwana Mungu wa majeshi , Yehova Yire, Bwana atakayetupatia sadaka …….muulize namna atakavyoifanya.Nazungumza kuhusu usimamizi wa utele.(walikuwa na miaka saba ya shibe iliyokuwa inakuja ) kile tukifanyacho utele unapotujia ndicho kitaleta tofauti njaa itujiapo.

Usifikilie hutakuwa na wakati wa njaa maishani mwako kwa sababu itakupata.Ni katika hiki kipindi cha njaa hututathmini kama tunamwamini ama tunaamini kile tunachomiliki.

Hatuoni ubahili wowote katika mpango ambao Mungu alimpa Yusufu .Kile tunachokiona ni usimamizi mzuri.Leo tunahakika kuwa asilimia kumi ni ya Mungu , asilimia kumi tunaiweka akiba na kutoka pale tunagharamia chochote tunataka kufanya.Hata hivyo omba usitumie pesa kufanya mambo tu.

Tunapopitia ordha mbalimbali, tutapata vitu vingi tunavyovitaka ,na kuanza kuwaza,"Nataka kila kitu".Tungemuuliza Mungu na kumpa nafasi aielekeze njia yetu , angetuonyesha kile tunachohitaji.

Huu ni usimamizi mzuri chini ya uongozi wa Mungu, katika Mwanzo 47, tunaona vile Yusufu alifanya wakati ule.Tunapata kuona jinsi mtu akiongozwa na Roho wa Bwana anavyoweza kusimamia na kutunza alichokarimiwa.

"*Yusufu akawaambia watu , angalieni nimewanunua leo, nyinyi,na nchi yenu , kuwa mali ya Farao, basi mbegu zenu ni hizi, pandeni katika nchi yenu*".(Mwanzo 47:23)

Unatakiwa kuichukua mbegu na kipanda katika nchi.Usitalajie kuuona muujiza wa kifedha maishani mwako kutoka kwa Bwana mpaka upande mbegu.

*"Itakuwa wakati wa mavuno mtampa Farao sehemu ya tano , na sehemu nne zitakuwa zenu wenyewe, kuwa mbegu ya nchi ,na chakula chenu na chakula cha waliomo nyumbani mwenu, na chakula cha watoto wenu .Wakasema umetulinda hai ,na tuone kibali machoni pa bwana wetu,nasi tutakuwa watumwa wa Farao*"(Mwanzo47:24-25).

Mambo yalibadilika lakini usimamizi mzuri ndio ulisababisha mabadiliko haya.

"Yusufu akaifanya sheria kwa habari ya nchi ya Misri hata leo ,ya kwamba sehemu ya tano iwe mali ya Farao.Ila nchi ya Makuhani tu haikuwa mali ya Farao"(Mwanzo 47:26).

Mpango wa Yusufu ndio ulikuwa mpango wa Mungu kuuauni ulimwengu wakati ule.Unaona kuwa kibali cha Mungu kilisababisha Yusufu kufika cheo cha juu bila kujali alikuwa nani.Kulikuwa na vipindi vya njaa maishani mwake pia.Mathalani aliuzwa na nduguze utumwani,aliwekewa mashtaka ya uongo na kufungwa jela.Hata hivyo Mungu kila wakati alimfaulisha ili mpango wake utimie wa kuuokoa ulimwengu wakati ule.

Njia ya pili ya kufungua muujiza wa kifedha katika maisha yako ni:

<u>KUONDOA HOFU NA MASHAKA NA KUPANDA MBEGU</u>

Yafikirie maisha ya Isaka, Alirithi hulka zingine za babake.Alihofia maisha yake alipoingia nchi ngeni.Unapoingia katika hali ya hofu na shaka kuhusu maisha yako na jinsi utakapoishi, inakufanya usipige hatua mbele Unajiondoa nakuwa bahili.Hutaweza kuwa mkarimu kwa sababu unaogopa kwa ajili ya maisha yako,hali yako ya usoni,jamii yako na jinsi utakavyokidhi mahitaji yako (kile utakachokula, kunywa na kuvaa,n.k)

Katika Mathayo 6 Yesu anasema tusisumbukie mambo hayo ."Bali tutafuteni kwanza ufalme wake , na haki yake,na hayo yote mtazidishiwa"(Mathayo 6:33) kwa nini? Kwa maana Mungu atakukarimia.Atatengeneza njia.

Ondoa hofu na mashaka ukitaka omba Mungu msamaha sema"Bwana nisamehe kwa kuwa na hofu kuhusu maisha yangu .Nisamehe kwa kijihofia.

Mfalme alimwambia Isaka "Amgusaye mtu huyu au mkewe atauawa. Hivyo hakuhofia maisha yake ama familia yake.

“Isaka akapanda mbegu katika nchi ile…………..”(Mwanzo 26:12).Nataka uone umuhimu wa jambo hili.Kulikuwa na njaa wakati Isaka alipanda mbegu zake.Hakuna akuzaye mimea mizuri wakati wa njaa!Lakini watu wa Mungu hufanya hivyo kwa sababu Mungu ndiye husababisha mimea kukuwa.Mungu ndiye akarimiaye hata wakati ambapo ulimwwengu unapitia hali ya ukosefu. Kwake hakuna ukosefu wowote .Naye amtumainie Mungu haogopi ukosefu pia.

Mungu anawataka watu wake wamtumainie na kumtafuta maana anaweza kuleta ongezeko kwa njia yoyote ile atakayo.Atatupa mpango.Tunatakiwa kuwa wasimamizi wenye hekima.(hoja nambari moja)Natuondoe hofu na mashaka kuhusiana na kile tunachokuwa nacho kwa ajili ya siku zijazo.(hoja ya pili

1. Isaka alipanda mbegu katika nchi ile ,akapata mwaka ule vipimo mia kwa kimoja.(Mwanzo 26:12)

Katika mwaka ule wa njaa , Isaka akaondoa hofu na mashaka .Alichukuwa hatua ya kupanda mbegu zake .Pia katika mwaka ule ule akavuna vipimo mia kwa kimoja “Bwana akambariki”(mwanzo 26:12)

Kama watu wa Mungu inatubidi kizitarajia baraka za Bwana tunapofanya alisemalo.

Nasisitiza kuwa njia ya pili ya kuifungua miujiza ya kifedha ni kuondoa hofu na mashaka na pia kupanda mbegu .Utakosa kuyaona mavuno ikiwa hautapanda chochote.Ukikosa kutoa chochote katika kazi ya Bwana usitalajie kuona mimea inayo kua ikibarikiwa na Mungu .

Unaweza kuona mimea ikinawri lakini kuwe na vizuri lakini kuwe na vijavyo kuiba.Tunataka mimea ibarikiwe na Mungu ambapo hatutaibiwa na mwizi.Kilichobarikiwa na Bwana utakifurahia.(Mhubiri 5:19)

Yaangalie kwa makini yasemwayo katika Mwanzo 26:13-14

*“Na mtu huyo akawa mkuu akazidi kustawi ,hata akawa mkuu sana.Akawa na mali ya kondoo na mali ya ng’ombe, na watumwa wengi.HaoWafilisiti wakamhusudu”.*

Watu huwainukia walio na kibali cha Mungu kwa sababu wanawahusudu .Usijali kuhusu hayo wapende watu nakuendelea na maisha .Baraka za Mungu zitaendelea kadiri unavyoendelea kutenda alisemalo”.

“Abimeleki akamwambia Isaka,Utoke kwetu maana wewe una nguvu sana kuliko sisi(Mwanzo26:16)

Napenda mstari huu ,nilijawa na furaha wakati nilipousoma na kuelewa .Nikasema”Bwana hivi ndivyo nataka watu waseme kunihusu”.

Walikuwa wakisema ,”Mungu wako ana nguvu sana”,Naamini kuwa ulimwengu watasimama na kuona wakati ambapo watu wa Mungu wamebarikiwa kilingana na neno lake .Wataka kumjua Yule Mungu asababishaye baraka hizi katika maisha yako.

Tuangalie hatua za kuifungua miujiza ya kifedha ya Mungu katika maisha yako .

1. Usimamizi wa hekima chini ya uongozi wa mungu.
2. Kuondoa hofu na mashaka na kupanda mbegu.

Njia ya tatu ya kufungua miujiza ya kifedha ni:

<u>BIDII NA UCHAPAJI KAZI</u>

Usitarajie Mungu atakupatia chochote bure.Haitendeki jinsi hiyo .Tuna mfano mzuri wa Yakobo.

Yakobo alifanya na kumchapia kazi Labani ili awaoe mabinti wake Labani.

*"Akamwambia umejua jinsi nilivyokutumikia ,na jinsi wanyama wako walivyokuwa kwangu. Maana mali yako ilikuwa haba kabla sijaja, nayo imezidi kuwa nyingi ,Bwana akakubariki kila nilikokwenda.Basi sasa nitaangalia lini mambo ya nyumba yangu mwenyewe?"(*Mwanzo 30:29-30)

Hii inamaanisha nimekufanyia kazi, angalia vile ambavyo Mungu amekubariki kutokana na bidii na utunzaji wangu.Mungu amekubariki kupitia kwangu." Ungetaka kumwambia mwajiri wako maneno kama yale?

Yusufu alikuwa mtu wa aina ile kama tulivyoona hapo awali.Popotealipoenda, watu walitambua kuwa baraka za Mungu zilikuwa juu yake na alibariki kila nyumba alomoishi.Yakobo alifanana naye.

Alimwendea Labani kwa maneno haya"Wajua jinsi nilivyojibidiisha na kuchapa kazi,jinsi nilivyokushughulikia na kufanya lile nilipaswa kulifanya".

Katika AganoJipya insemekana Mungu atakuamini kwa machache na ukiaminika kwa yale atakuweka juu ya mengi .(Mathayo 25:21)ukiwa mwaminifu kwa kile ulicho nacho naye Mungu atakuongezea usitarajie muujiza wa kifedha hadi uwe mwaminifu katika kile ulicho nacho .(Luka 16:10).

"*Yakobo akawaambia wake zake,naona uso wa baba yenu ,kwamba hanitazami vyema kama jana na juzi .Lakini Mungu wa baba yangu amekuwa pamoja nami".(Mwanzo 31:5)Ukitaka kuona muujiza wa kifedha katika maisha yako , lazima mjue Mungu wa baba zako yu pamoja nawe*.

"Nanyi mmejua ya kwamba kuwa nguvu zangu zote nimemtumikia baba yenu."(Mwanzo 31:5).Unataka kuweza kusema"Nimeweka kila kitu nilichikuwa nacho katika jambo lile .Nimefanya nililopaswa kufanya kwa utukufu wa Mungu ".(Wakolosai3:23)

"Yakobo aliendelea ……………………., na baba yenu amenidangaya , akabadili mshahara wangu mara kumi",(Mwanzo 31:7)Mtu huyu alihitaJi muujiza wa kifedha katika maisha yake.kila alipofanya jambo ili afanikiwe Labani alikuja kulibadilisha na kumnyang'anya .Je , umewahi kuwa katika hali hii?Chochote kilichoingia kilirudi kilichotoka, hata wakati ambapo unajua unafanya kile Mungu akitakacho .Hadithi hii ni mfano mzuri wa muujiza wa kifedha.

Tazama hata Labani aliweza kubadilisha mshahara wa Yokobo mara kumi,Yakobo alikuwa mwaminifu kwa Mungu na Labani.Huyu ni mtu ambaye hangeondoka bila Baraka za Mungu na zile ambazo Mungu alipenda kumpatia.

"Aliposema,' Walio na madoadoa watakuwa mshahara wako' Wangu wote wakazaa madoadoa.Aliposema,' Walio na miliia watakuwa mshahara wako' ,ndipo wanyama wote wakazaa wenye milia.Hivi ndivyo Mungu atamnyang'anya mali yote baba yenu ,na kunipa mimi".(Mwanzo 31:8-9)

Unaweza kuuona muujiza wa kifedha ambao Mungu alikuwa akifanya .Yakobo aliendelea kuwa mwaminifu kwa Mungu na akawa na nia nzuri kwa Labani(ambayo ni muhimu sana )Mungu aliendelea kumtendea Yakobo.

"Ikawa wakati wele wanyama walichukua mimba,niliinua macho yangu nikaona katika ndoto natazama mabeberu waliowapanda hao wanyama walikuwa na millia, madoadoa na marakaraka.Na malaika wa Mungu akaniambia katika ndoto 'Yakobo 'Nikasema mimi hapa'Akasema basi inua macho yako ,ukaone mabeberu wote wanaopanda hao wanyama wote wana milia,na madoadoa na marakaraka,maana nimeona yote aliyokutendea Labani . Mimi ni Mungu wa Betheli huko ulikotia mafuta nguzo na kuniwekea nadhiri.Sasa ondoka toka katika nchi hii urudi mpaka nchi uliozaliwa".(Mwanzo 31:10-13)

Na mali yamkosaji huwa akiba kwa mwenye haki,(Methali 13:22,Ayubu 27:16-17,mhubiri2:26)

Hata wakati ambao waovu wanapodanganya Mungu atabariki watu wake.

Tazama tena

1. Usimamizi wenye hekima chini ya uongozi wa Mungu .
2. Kuondoa hofu na mashaka; kupanda mbegu.
3. Bidii na uchapaji kazi.

Njia ya nne ya kufungua muujiza wa kifadha ni:

KUMUENZI MUNGU KWA ONGEZEKO

Natumtazame Abramu katika Mwanzo 14.Baada ya kushida vita, Melkizedeki mfalme wa Salemu alimjia (Yesu anaitwa kuhani anayefananishwa na Melkizedeki ambaye hudumu milele).

*"Na Melkizedeki mfalme wa Salemu akaleta mkate na divai , naye alikuwa kuhani wa Mungu aliye juu sana .A kambariki akasema,'Abramu na abarikiwe na Mungu aliye juu sana ,muumba mbingu na nchi .Ahidimiwe Mungu aliye juu sana .aliyewatia adui zako mikononi mwako'.Abramu akampa fungu la kumi la vitu vyote'*.(Mwanzo 14:18-20)

Kila wakati tunapopata muujiza wa kifedha au baraka hatuna budi kumshukuru Mungu.Tunatoa fungu la kumi pamoja na sadaka ili kumuenzi Mungu na kumshukuru kwa sababu ya baraka za kwetu.Tunapompatia tunamwambia ,"Tunakutumaini na kushukuru Bwana"

Bwana aliniambia wakati mmoja "Watu wenye shukurani hutoa kwa kazi yangu ,watu wenye shukurani hunienzi kwa kutoa kwao."Wanamshukuru Mungu kwa sababu ya ukarimu wake .

Fungu la kumi ni sehemu ya kumi kwa mia ya mapato yote uyapatayo .(Malaki 3:8-12,Mwanzo 14:18-20,Mithali 3:9-10)Tuyashughulikie kwanza yale yanayotakiwa kushughulikiwa kwanza. Tazama neno halisemi Abramu hakutoa ili alipe kodi au afanye jambo lingine.Alimpatia Mungu kwanza ,"Basi vya Kaisari mpeni kaisari ,na vya Mungu mpeni Mungu "(Luka 20:25).

Katika nchi hii Mungu ametubaliki vya kutosha unapomuenzi Mungu naye atakuenzi kupitia kaisari (serikali)Usiaibike kujilipia kodi yako mwenyewe unapotoa katika kazi ya Bwana. Mungu anafanya hivyo kupitia viongozi wanaotutawala.

Tuangalie kwa makini vile Abramu alifanya kutokana na shukurani zake kwa Mungu .Alimpatia Mungu sehemu ya kumi ya kila kitu.

*"Mfalme wa Sodoma akamwambia Abramu ,nipe mimi hao watu , na hizo mali uchukue wewe ,'Abramu akamwabia mfalme wa Sodoma ,'Nimeinua mkono wangu kwa Bwana,Mungu aliye juu sana muumba wa mbingu na nchi ya ya kuwa sitatwaa uzi wala gidamu ya kiatu wala chochote kilicho chako , usije ukasema ,'nimemtajirisha Abramu,'*(Mwanzo 14:21-23)

Mungu wala si mwanadamu hutajirisha hubariki Kumbukumbui la Torati 8:17,Mhubiri5:19,2 Wakorinitho 9:8-11.

Anatupatia uwezo wa kuwa tajiri,usiwahi fikiria ni kwa uwezo wako wala hekima yako, mipango yako mizuri, kuwaza haraka au bahati. Mungu huwapa hekima na uwezo wa kupata utajili wale wanaomwamini na kumtii.

Hata hivyo hatuna budi kumuenzi Mungu kwa kile alichotupa.Hatowapa muujiza wa kifedha na baraka zake watu ambao hawatamuenzi .umewahi kuwa mahali ambapo unatamauka kila wakati?Ulikaribia kupata upenyo lakini unaonekana kukuponyoka .Jambo hili linamfanyika kwa sababu kuna mwizi anayeiba lakini Mungu ametukarimia.

Je?Mwanadamu atamwibia Mungu ?Llakini ninyi mnaniiba mimi.(Malaki 3:8)

Hivi ni kusema, je,kuna yeyote anayeweza kumwibia Mungu?Lakini anaedelea kusema ,lakini ninyi mnaniibia"Kwa hivyo kuna watu leo ambao wanamwibia Mungu .

"*Lakini ninyi mwasema ,'Tumekuibia kwa namna gani?Mmeniiba kwa zaka na dhabihu.Ninyi mmelaaniwa kwa laana;maana mnaniibia mimi,naam,taifa hili lote.Leteni zaka na dhabihu kamili ghalani ,ili kiwemo chakula katika nyumba yangu mkinijaribu kwa njia hiyo asema Bwana wa majeshi .Na mataifa yotewatawaiteni heri , maana mtakuwa nchi ya kupendeza sana asema Bwana wa majeshi* (Malaki3:8-12)

Nakutahadharisha leo ikiwa hutoi fungu la kumi

1. Unakosa kumtii Mungu
2. Unamwibia Mungu
3. Unakosa kuruhusu muujiza wa kifedha utendeke katika maisha yako.usitarajie muujiza wa kifedha ukikosa kutoa fungu la kumi na sadaka.

Huenda jambo hili limewahi kutendeka katika maisha yako.ulikosa kumuenzi Mungu kwa kutoa fedha zako au kumpa shukurani.Ulilopata kujua tena ni kuwa jambo Fulani lilitendeka na sehemu ya pesa zako zikatumika pale.Jambo lingine likatendeka au likaharibika na sehemu ya pesa ikatumika pale.

Yesu husema "Mwizi haji ila aibe na kuchinja na kuharibu mimi nalikuja ili wawe na uzima ,kasha wawe nao tele .(Yohana 10:10)

Anazungumzia kuhusu pepo wanaojaribu kuiba fedha zetu wanaosababisha vitu kuharibika .Mungu anasema nitasimama dhidi yao .Sasa unaweza kusimama na kusema ,"katika jina la Yesu,Shetani natoa fungu la kumi na huwezi tena kusababisha uharibifu wa mali zangu.Nitatumia kwa ukalimifu vyote ulivyonipa Mungu mpaka vizeeke.(kweli, sisi hupanga, pia vile tutakavyohifadhi kile tulichopewa na Mungu .Usitarajie gari litaendelea kutumkia ukikosa kubadilisha mafuta )

Ni muhimu sana kuona kila kitu ulicho nacho kimetoka kwa Bwana .Hii inamaanisha kuwa hujakimiliki, ni mali ya Mungu .Wewe ni mtunzaji wa ukarimu wa Mungu . Acha Shetani ajaribu kumwibia Mungu.

Unapotoa fungu la kumi pamoja na sadaka ,unamuenzi Mungu na kumwambia,"Mungu hii ni mali yako"Ni sadaka ya shukrani kwa kupewa mwanya wa kuitunza kuitumia na kuifurahia. .Umegundua kuwa Mungu anataka tufurahie kile alichotupatia.(Timotheo 6:17-20).

"*Mheshimu Bwana kwa mali yako na kwa malimbuko ya mazao yako yote.Ndipo ghala zako zitakapojazwa kwa wingi .Na mashinikizo yako yatafurahika kwa divai mpya* (Mithalli 3:9-10).

Tunza; malimbuko ya mazao yako yate sio mapato yaliyosalia lakini ni jumla ya mapato yote .Huku ni kutenda kwa imani.Ghala zako zitajazwa kwa wingi ........"Wapeeni watu vitu nanyi mtapewa kipimo cha kujaa na kushidiliwa ,na kusukukwa sukwa hata kumwagika ......"(Lluka 6:38)

Katika njia hii tunazungumza kuhusu imani .Tayari tumeondoaa hofu na mashaka ,tumeachwa na nini?Kumwamini na kumtumaini Mungu .”Iwapo amesema ,hatalitenda? Iwapo amenena ,hatalifikiliza?”(Hesabu 23:19)

Muenzi Mungu kwa ongezeko lako bali usitarajie muujiza wa kifedha bila kumuenzi vile.

Tazama tena

1. Usimamizi wenye busara chini ya uongozi wa Mungu
2. Kuonda woga na mashaka na kupanda mbegu.
3. Bidii na uchapaji kazi.
4. Kumuenzi Mungu kwa ongezeko.

Hatua ya tano katika kuufungua muujiza wa kifedha maishani mwako ni:

<u>KUWA NA MOYO MNYENYEKEVU WENYE KUTUBU NA KURITHIKA KWA KILE ULICHO NACHO</u>

Ndipo Ayubu akamjibu Mungu na kusema ,”Najua ya kuwa waweza kufanya mambo yote na ya kuwa makusudi yako hayawezi kuzulika.Ni nani huyu afichaye mashauri bila maarifa? Kwa maana nimesema maneno nisiyoyafahanu .Mambo ya ajabu ya kunishida mimi nisiyoyajua.”(Ayubu 42:1-3)

Kuna watu leo ambao huzungumza mambc wasiyowafahamu.Wanahitaji kuangalia ni njia gani Mungu ayasemayo na kutenda wanalopaswa kufanya.Usisongee kutokana na kutojua kuhusu utakayoyatenda au kutoyatenda Mungu ikiwa hujasoma Biblia.Pia watu wamesoma Biblia bila kufahamu inalolisema.

Wanaweza kufikiria ,maskini Ayubu, nafanana tu na  maskini Ayubu, Hebu nikwambie nataka kufanana na Ayubu –lakini si Yule Ayubu wanaomzungumzia.Nataka kuwa Ayubu ambaye anazungumziwa na Biblia katika sura ya 42. Tazama kilichotendeka.”Sikiliza,nakusihi,nami nitanena;nitakuuliza neno,nawe uniambie.Nlikuwa nimesikia habari zako, kwa kusikia kwa masikio; bali sasa jicho langu linakuona kwa sababu hiyo najichuklia nafsi yangu na kutubu katika mavumbi na majivu”(Ayubu 42:4-6)

Watu wengi wanamlaumu Mungu kwa kile kinachofanyika maishani mwao .Hawaelewi kuwa Mungu anawawazia mazuri wala si mabaya.Mawazo ya kuwapa tumaini siku zao za mwisho (Yeremia 29:11)

Ikiwa uko katika hali ile ya kumlaumu Mungu  na ungetaka kuufungua muujiza wa kifedha ,njia ya tano ni kunyenyekea mbele ya Mungu na kutubu.Hii inamaanisha kumwomba Mungu msamaha na kukoma kumlaumu  Mungu na wengine pia kuacha kunena kinyume na ahadi za Mungu.Ridhika na kushukuru kwa hali uliyomo .(1 Timotheo 6:6-12, Wafilipi 4:9-10) Shukuruni kwa kila jambo(1 Wathesalonike 5:18) Mungu ni mkuu kuliko hali zetu na atautenda muujiza wa kifedha kwa ajiri yako.

Ayubu alihitaji muujiza wa kifedha maana alipoteza mali yake yote.Bwana alialimwamuru awaombee rafikize(Mstari 10).Angalia kilichotendeka.”Bwana naye akampa Ayubu mara mbili kuliko hayo aliyokuwa nayo kwanza.”(Ayubu 42:10)

Maskini Ayubu ningetaka tu kufanana naye.Na wewe?Neno linasema Mungu aliponya nakumpa maradufu kuliko hayo alikuwa nayo kwanza.Alikuwa tajiri wa kutajika siku hizo kwa sababu ya baraka za Mungu katika maisha yake.Mungu alimpa maradufu.

“*Ndipo wakamwendea nduguze wote,waume kwa wake nao wote walijuana naye hapo zamani,wakala chakula pamoja naye katika nyumba yake, nao wakamlilia na kumtunza moyo katika habari za uovu huo wote Bwana aliouleta juu yake, kila mtu akampa kipande cha fedha, na pete ya dhahabu kila mmoja.”(*Ayubu 42:11)Ungetaka rafiki zako wote kukujia na kukupa fedha na dhahabu.

“*Basi hivyo Bwana akaubarikia huo mwisho wa Ayubu zaidi ya mwanzo wake ,naye alikuwa na kondoo kumi na nne elfu, na ngamia elfu sita na jozi za ng’ombe elfu , punda elfu .Tena alikuwa na wana waume saba , na binti watatu ……….katika nchi hiyo yote hawakuwapo wanawake waliokuwa wazuri kama hao wana wa Ayubu na baba yao akawapa urithi kati ya ndugu zao wana waume. Kisha baada ya mambo hayo Ayubu akaishi miaka mia na arobaini , naye akawaona wanawe na wana wanawe, hata vizazi vinne.Basi Ayubu akafa mzee sana mwenyewe kujawa na siku*.(Ayubu 42:12-13, 15-17)

Ayubu hakuishi maisha yake yote katika hali hiyo ya umasikini.Yamkini miezi sita tu. Umewahi kuwa katika HALI kama ile?Mungu alimsalimisha kutokana nayo . Alimpa Ayubu miaka mia arobaini zaidi (Tazama pia Zaburi 34:17-19; 2 Timotheo 4:18;1 Wakorintho 10:13)

Ukitazama kwa uangalifu sura ya kwanza ya kitabu cha Ayubu utaona kuwa Mungu hakusababisha uovu uliompata Ayubu maishani mwake .Shetani pamoja na Ayubu mwenyewe waliusababisha. “Maana jambo hilo nichalo hunipata nalo linitialo hofu hunijia “(Ayubu 3:25)

Ayubu alimfungulia shetani mlango naye Shetani akaingia .Hata hivyo mkono wa Mungu ulimlinda na akasema “yote aliyo nayo yamo katika uwezo wako , lakini usinyoshe mkono wako juu yake yeye mwenyewe.”

Kuwa hai ni baraka ya Mungu ukikosa uhai huwezi kubarikiwa katika dunia hii .utabarikiwa katika dunia mpya pamoja na Yesu .Mungu anawezaje kutenda muujiza wa kifedha ukiwa mfu . Hawezi.

Mungu alikusudia nini kwa Ayubu alitaka kumbariki? .Alitaka kumfanya mfano ili ulimwengu uone jinsi Mungu anavyoweza kubariki na kumfanikisha mwenyewe moyo mnyenyekevu na unaotubu na mwenyewe kuridhika katika maisha yake.(Malaki3:12)

*“Walakini utauwa pamoja na kuridhika nii faida kubwa*”(Timotheo6:6)Ulikuja ulimwenguni bila chochote na utarudi bila kitu.Usipende pesa ama utajitia mwenyewe katika mtego.

Hii nikusema kuwa usitafute miujiza ya kifedha kutoka kwa Mungu kwa ajili yako mwenyewe.Tafuta ili uendeleze ufalme wa Mungu.Sijawahi kuona Mungu akikosa kulijibu ombi wakati watu wameomba sadaka ili wampe Mungu.Mungu hakarimia kwa sababu anataka kazi ya ufalme wake izidi kuendelea kwa utukufu wake tena watu wake washughulikiwe.

1Timotheo 6:17-19 hutwambia vile tunavyotaakiwa kufanya na utajiri wakati tuupatapo .Tunatakiwa kutenda mema tuwe tayari kutoa mali zetu tushirikiane na wengine kwa moyo na pia tusiutumainie utajiri usio yakini .Tunatakiwa kimuenzi Mungu na kumshukuru kwa sababu ya ukarimu wake na tuwe baraka aliyoikusudia Mungu humu duniani.

Tuangalie tena

1. Usimamizi wenye hekima chini ya o ongoziwa Mungu
2. Kuondoa hofu na mashaka
3. Bidii na uchapiji kazi
4. Kumuenzi Mungu kwa ongezeko

5. Kuwa na moyo mnyenyekevu, wenye kutubu na kuridhika kwa kile ulicho nacho.

Ukitaka kuona muujiza wa kifedha katika maisha yako basi tekeleza hatua ya sita .

TAFUTA HEKIMA YA MUNGU

Tuyaangalie maisha ya Sulemani kama kijana. Babake, Daudi alikuwa amekufa naye Mungu akamtokea. *"Bwana akamtokea Sulemani katika ndoto ya usiku; Mungu akamwambia, omba uatakalo nikupe*!"

(1 Wafalme 3:5)

Waza kuhusu jambo hili. Alikuwa kijana tu wakati ule. Mungu akamtokea na kumwambia, 'omba utakalo nikupe' ungetaka Mungu kukutokea na kukuliza hivyo?

Katika Yesu Kristo, Mungu amefanya hivyo. "*Nanyi mkiomba lolote kwa jina langu, hilo nitafanya" (Yohana 14:13) kwa nini tusitarajie miujiza ya fedha*? Tazama kilichotendekea Sulemani.

"*Sulemani akasema, "umemfanyai mtumwa wako Daudi baba yangu fadhili kuu, kadri alivyoenenda mbele zako katika kweli, na katika haki na katika unyofu wa moyo pamoja nawe; umemwekea na fadhili hii kubwa, maana umempa mwana wa kuketi kitini pake. Kama ilivyo leo. Na sasa ee Bwana, Mungu wangu, umenitawaza niwe mfalme mimi mtumwa wako badala ya Daudi baba yangu; nami ni mtoto mdogo tu; sijui inipasavyo kutoka wala kuingia*"

(1 Wafalme 3:6-7)

Sulemani alikuwa na shauku ya unyofu katika usimamizi ili aweze kushughulikia amana ambayo Mungu alimwaminia. Katika Agano jipya, Yesu alisema kuwa tukikosa kujua jinsi ya kutumia pesa kwa njia ya hekima, basi hatutaweza kuaminiwa kwa amana na mali ya kweli. (Luka 16:11)

*"Na mtumwa wako yu katikati ya watu wako uliowachagua, watu wengi wasioweza kuhesabiwa, wala kufahamiwa idadi yao, kwa kuwa ni wengi. Kwa hivyo nipe mimi mtuwa wako wa adili niwahukumu watu wako, na kupabanua mema na mabaya."*

(1 Wafalme 3:8-9)

Tunahitaji kuenda mbele za Mungu na moyo kama ule (Nimejifunza mengi ya maombi yangu kutokana na neno la Mungu. Nimegundua ni maombi gani yanayobarikiwa.Hayo ndiyo maombi nitumiayo) Mungu alibariki ombi la Sulemani nami nimekuwa nikiliomba tangu nilipokuwa mvulana mdogo.

*"Bwana nipe mimi mtumwa wako moyo wa adili niwahukumu watu wako na kupambanua mema na mabaya"* nami huongezea, "Neema(uwezo) pia, kufanya yaliyo ya haki na kuyaondokea yaliyo maovu" Sulemani hakuomba hivyo katika ombi lake na alifanya dhambi baadaye. Ni jambo moja kujua yaliyo mema na mabaya na ni jambo lingine kutenda yaliyo mema na kuyaondokea mabaya.

*"Neno hili likwa jema machoni pa Bwana, ya kuwa Sulemani ameomba hili.*" (1 Wafalme 3:10)

Kwa nini Mungu alipendezwa na jambo hili? Kwa sababu Sulemani hakupendelea nafsi yake. Alimpa Mungu na watu wake nafasi ya kwanza katika moyo wake. Huuhitaji miujiza ya kifedha kwa manufaa yako mwenywe. Unahitaji kwa ajili ya Mungu. Mungu atawapa watu pesa anaojua anawaaminia.

“*Mungu akamwambia, ‘Kwa kuwa umeomba neno hili wala hukujitakia maisha ya siku nyingi, wala hukutaka utajiri kwa nafsi yako, wala hukutaka roho za adui zako, bali umejitakia akili za kujua kuhukumu, basi tazama, nimefanya kama ulivyosema. Tazama nimekupa moyo wa hekima na wa akili, hata Kabla yako hapakuwa mtu kama wewe wala baada yako hatainuka mtu kama wewe nimekupa mali na fahari ,hata hapatakuwa na mtu katika wafalme kama wewe siku zote*”(1 wafalme 3:10-13)

Hili ni jambo la kufurahisha .Njia ya sita ya kufungua miujiza ya kifedha ni kutafuta hekima ya Mungu .Ukitafuta hekima ya Mungu basi Mungu anasema atafanya nini ?Neno linasema atakupa kile ambacho hukuomba .Hakitakuwa kibaya .Hebu nikwambie ni nini.”mali na fahari”(1 Wafalme 3:13)

Mungu anasema atakupa atakupa mali na fahari hata ikiwa hukuomba mambo yale.Ulitamani kutafuta hekima kutoka kwa Mungu wala hukujitakia mambo yale kwa hivyo atakupa mali na Fahari .Ondoa mawazo ya umasikini.

“*Hata hapatakuwa na mtu katika wafalme kama wewe, siku zako zote.Nawe ukienda katika njia zangu na kuyashika mausia yangu , na amri zangu , kama babako Daudi alivyokwenda ,basi nitazifanya siku zako kuwa nyingi*.”(1 Wafalme 3:13-14)

Mali na fahari kwa upande mmoja , maisha marefu upande mwingine.Je dunia yote inatufuta nini?Mali na maisha marefu .Mungu ndiye pekee hutupatia akiambatanisha na baraka ili uweze kufurahia. Anataka kukufanyia hivyo.

Nanaamini na pia ni neno la Mungu kuwa ikiwa amekukarimia chochote,samamia vizuri na usiishi nje ya kile ulichopewa wakati wa kufanya kazi kwa nguvu ni wakati wa utele .

Kuchakuro hujiweka akiba ya kile wawezao kwa sababu wanajua msimu wa kipupwe unawadia nao ardhi haitatoa chochote,wao hufanya kazi kwa nguvu.

*“Mheshimu bwana kwa mali mbuko ya mazao yako yote .Ndipo ghala zako zitakapojazwa kwa wingi na mashinikizo yatafurikadivai mpya*.”(Mithali 3:9-10)

Mungu hutaka watu wake watambuliwe wanampatia utukufu Mungu atawainua (kuinuliwa kunatokana na Mungu)

“Njia zake ni njia za kupendeza sana,na mapito yake yote ni  amani .Yeye ni mti wa uzima kwao wamshikao sana .Ana heri kila mtu ashikamanaye naye”(Mithali 3:17-18)

Tuangalie upya  hatua zote sita za kufungua miujiza ya kifedha ya Mungu

1. Usimamizi wenye hekima chini ya uongozi wa Mungu
2. Kuondoa hofu na mashaka na kupanda mbegu
3. Bidii na uchapaji kazi
4. Kumuenzi Mungu kwa ongezeko-fungu la kumi na sadaka
5. Kuwa na moyo myenyekevu ,wenye kutubu, kuridhika na ulicho nacho.
6. Kutatuta hekima ya Mungu

© 1990, Dr. Randy Brodhagen, Glory To God Ministries International™, all rights reserved